# MKATABA WA MAUZO YA KIWANJA

KATI YA

GOODLUCK PAUL SAMWEL

NA

AL HASEEB JEWELRY LIMITED

Scanned with CamScanner

JAMUHURI YA MUUNGANO YA TANZANIA

---

MKATABA WA MAUZO YA KIWANJA

Mapatano haya yamefanyika leo siku ya tarehe 23 mwezi wa Feb Mwaka 2023

KATI YA

GOODLUCK PAUL SAMWEL wa sanduku la Posta nambari 36619 DAR ES SALAAM, Tanzania ambaye atajulikana kama 'MUUZAJI".

NA

AL HASEEB JEWELRY LIMITED wa sanduku la Posta nambari 20824 DAR ES SALAAM (ambaye hapa atajulikana kama "MNUNUZI" kwa upande mwingine.

KWA KUWA, MUUZAJI ni mmiliki halali wa kiwanja kilicho pimwa na kinachotambulika, kama Kiwanja Namba P19921" katika eneo la KISARAWE II, Wilaya KIGAMBONI ndani ya Jiji la Dar Es Salaam ambapo Kiwanja hicho kinaukubwa wa mita za mraba (17203 sqm). Kiwanja hichi kimepimwa kwaajili ya matumizi ya kiwanda.

KWA KUWA Muuzaji anania ya kuuza kiwanja kilichotajwa hapo juu pamoja na viambatanisho vilivyomo katika kiwanja hicho (ambacho hapa kitajulikana kama "KIWANJA") kwa jumla ya thamani ya *fedha za Tanzania shilingi Milioni Miamoja na thelathini tu (130,000,000/=)* na mnunuzi yuko tayari kununua kiwanja hicho kama jinsi kilivyo.

HIVYO BASI, MUUZAJI kwa hiyari yake mwenyewe amekubali kumuuzia MNUNUZI kiwanja hicho kilichotajwa hapo juu bila ya vikwazo vyovyote na katika hali kama jinsi kilivyo, na pande zote mbili zimekubaliana kama ifuatavyo:-

Scanned with CamScanner

1. KWAMBA, MUUZAJI ni mmiliki halali wa kiwanja kilichotajwa hapo juu na anania ya kumuuzia MNUNUZI kwa makubaliano yaliyomo katika mkataba huu.

2. KWAMBA, kwamakubaliano ya pande zote mbili kiwanja hicho kitauzwa kwa jumla ya *fedha za Tanzania shilingi Milioni Miamoja na thelathini tu (130,000,000/=) ambazo zita tambulika kama fedha kwa ajili ya manunuzi ya kiwanja hicho"* ambapo malipo hayo ya fedha yatalipwa kwa awamu moja tu kama ambavyo pande zote mbili walivyokubaliana katika mkataba huu.

3. KWAMBA, malipo yaliyoainishwa katika aya ya 2 ambayo yametambulika kama *malipo ya fedha kwa ajili ya manunuzi ya kiwanja* katika mkataba huu, Ifahamike ya kwamba malipo hayo yamelipwa kwa awamu mmoja *tu* ambapo MUUZAJI amekiri kupokea kiasi hicho kwa tarehe ya leo ambayo mkataba huu pande zote mbili wameweka saini zao na kushuhudiwa na mwanasheria wao.

4. KWAMBA, malipo yote yafanyika kwa njia ya Benki tu na si vinginevyo kwenye akaunti Namba ifuatayo;-

   Akaunti Namba: 24510016525
   Jina la Akaunti: GOODLUCK PAUL SAMWEL
   Jina la Benki: NMB

5. KWAMBA, MUUZAJI anapaswa kutoa nyaraka zote za umiliki wa kiwanja hicho na kumpatia MNUNUZI mara baada ya Mnunuzi katika mkataba huu kukamilisha malipo yote ya manunuzi ya kiwanja hicho.

6. KWAMBA. MUUZAJI atapaswa kutoa ushirikiano na msaada pale utakapo hitajika katika uhamishajiwa jina la umiliki wa kiwanja hicho kutoka Jina lake kwenda kwenye majina ya MNUNUZI. Gharama za kuhamisha umiliki wa kiwanja hicho zitaghariwa na Muuzaji kama ambavyo pande zote mbili walivyokubaliana.

Scanned with CamScanner

7. KWAMBA, Muuzaji anathibitisha kuwa anahaki na mamlaka ya kuuza kiwanja kilicho tajwa hapo juu na kwamba kiwanja hicho hakina madeni wala vikwazo vyovyote.

8. KWAMBA, Kiwanja hicho kinauzwa kwa jinsikilivyo na utunzaji wowote ule utakuwa ni gharama ya MNUNUZI na kwamba MUUZAJI na MNUNUZI wote kwa pamoja wanatambua na kukubaliana hivyo.

9. KWAMBA, MUUZAJI anamthibitishia MNUNUZI wa kiwanja hicho kuwa hakina mgogoro wowote na wategemezi wake, warithi wake, Jamaa zake ndugu zake, familia yake na pia kiwanja hicho hakijawahi kuwekwa kama dhamana katika taasisi yoyote ya kibanki kwa lengo la kuchukua mkopo.

10. KWAMBA, MNUNUZI wa kiwanja hicho anakiri kwa hiyari yake mwenyewe bila kushurutishwa na mtu kuwa kiwanja hicho atakituza na kukifanyia maendelezo kwa mujibu wa sheria inavyomtaka.

11. KWAMBA, endapo katika mkataba huu MUUZAJI au MNUNUZI atakiuka aya yoyote na kupelekea hasara yoyote basi upande utakaoathirika na kitendo hicho utakuwa na haki ya kudai fidia kutokana na ukiukwaji huo uliofanyika na unaweza kupeleka madai yake katika mahakama yoyote yenye mamlaka katika kutatua mgogoro huo na pia unaweza kuvunja mkataba na kurudia katika hali kama ilivyokuwa mwanzo.

12. KWAMBA MUUZAJI na MNUNUZI wote kwa pamoja wanakubaliana kwamba iwapo mgogoro wowote utatokea kati ya pande hizi mbili, basi mgogoro huu utatatuliwa kwa mujibu washeria za Jamuhuri ya Muungano ya Tanzania kwa wakati huo zimetawala.

Makubaliano haya yamefanyika na kushuhudiwa na kama inavyoonekana hapa chini;

Scanned with CamScanner

Umeshuhudiwa na Umetiwa saini hapa Dar Es Salaam na GOODLUCK PAUL SAMWEL
Ambaye ninamfahamu/au ametambulishwa kwangu na ______
ambaye ninayemfahamu na kumshuhudia kwa tarehe ya leo tarehe 23 ,Mwezi Februari 2023.

MUUZAJI

MBELE YANGU

Jina NOEL J. SHANI
Saini
Anwani S.L.P 216 DSM
Wadhifa WAKILI

NOEL J. SHANI ADVOCATE NOTARY PUBLIC & COMMISSIONER FOR OATHS P.O. Box 262, DAR-ES-SALAAM

Umeshuhudiwa na Umetiwa saini hapa Dar Es Salaam na JOHNSON MOSES
Ambaye ninamfahamu/auametambulishwa kwangu na ______
ambaye ninayemfahamu na kumshuhudia kwa tarehe ya leo tarehe 23 ,Mwezi Februari 2023.

SHAHIDI WA MUUZAJI

MBELE YANGU

Jina NOEL J. SHANI
Saini
Anwani S.L.P 216 DSM
Wadhifa WAKILI

NOEL J. SHANI ADVOCATE NOTARY PUBLIC & COMMISSIONER FOR OATHS P.O. Box 262, DAR-ES-SALAAM

Scanned with CamScanner

AL HASEEB JEWELRY LTD. P.O. Box 20824 DAR-ES-SALAAM

Umeshuhudiwa na Umetiwa MUHURI WA KAMPUNI hapa Dar Es Salaam na AL HASEEB JEWELRY LIMITED Ametambulishwa kwang na
____________________
ambaye ninayemfahamu na kumshuhudia kwa tarehe ya leo tarehe 23 ,Mwezi Februari 2023.

____________________

MNUNUZI

Jina Hafeez-ur-Rahman Tariq
Saini [signature]
Anwani 20824
DSM
Wadhifa Mkurugenzi

Jina Mohammed Hassan Tariq
Saini [signature]
Anwani 20824
DSM
Wadhifa Mkurugenzi

MBELE YANGU

Jina NOEL J. SHANI
Saini [signature]
Anwani SLP 0216
DSM
Wadhifa NOTARY

NOEL J. SHANI ADVOCATE NOTARY PUBLIC & COMMISSIONER FOR OATHS P.O. Box 262, DAR-ES-SALAAM

Scanned with CamScanner